TANGAZO LA SERIKALI NA. 320 la tarehe 26/4/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA AFYA, LISHE NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA YA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya, Lishe na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali au leseni zitolewazo na Halmashauri;

"adha" maana yake ni hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara juu ya afya ya watu kwa ujumla;

"afya" maana yake ni hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na wala sio kutokua na ugonjwa au

ulemavu;

Sura ya 428 "afisa afya" maana yake ni afisa afya yeyote aliyesoma na kufaulu sayansi ya mazingira na kusajiriwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wataalamu wa Afya ya Mazingira;

"afisa lishe" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyesoma na kufaulu sayansi ya lishe ya binadamu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali;

"afisa mtendaji wa kijiji/mtaa" maana yake ni afisa mtendaji wa kijiji au mtaa aliyeajiriwa ndani ya Manispaa ya Tabora;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunyweka na binadamu isipokuwa dawa, hii ni pamoja na-

(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;

(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula;

(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula kama vile binzari na vingine vinavyofanana na hivi;

"chanzo cha maji" maana yake ni eneo lolote ambalo limetunzwa kwa ajili kua chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii;

"choo cha umma" maana yake ni choo kilichojengwa na Halmashauri au wakala wake au mtu binafsi au kampuni kwa matumizi ya umma na kuthibitishwa na Halmashauri pamoja na Baraza la Afya la mazingira;

"eneo la wazi" maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi

yaliyokusudiwa;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Tabora;

"hati ya usafi" maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hii kulingana na Sheria ya Afya ya Umma na kanuni zake;

Sura ya 99

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji kwa kuzingatia masharti ya Sheria ndogo hii au sheria nyingine zinazohusu mazingira;

"jengo la biashara" maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli za biashara;

"kaya" maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja au ndani ya chumba kimoja na kuishi kama familia na kula chungu kimoja au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"kelele" maana yake ni kero isababishwayo na sauti ambayo kwa asili inakataliwa au ile ambayo inaweza kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu au mazingira, sauti ya aina hii pia inaweza kubainishwa na kamati ya taifa na viwango kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa mazingira;

Sura ya 191

"kero" au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha -

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu.
(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi au kuleta kinyaa
(c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria ndogo hii;

"kuchakata taka" maana yake ni kuchambua, kuzitenganisha, kuzibadilisha na kuwa kitu kingine au kutoa zao jingine lenye manufaa kwa jamii;

"kuvuna miti" maana yake ni kufyeka, kukata au kung'oa miti au visiki katika misitu;

"mabwawa ya maji taka" maana yake mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kuchakata maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, kutoka vyooni, kutoka bafuni, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zozote za nyumbani, viwandani na kwenye taasisi mbalimbali;

Sura ya 123

"madini ya ujenzi" yanajumuisha aina zote za madini ya ujenzi yaliyoainishwa katika Sheria ya Madini;

"maji taka" maana yake maji yenye mchanganyiko wa kinyesi, mkojo, na maji kutoka masinki ya kuogea, kutema mate na kunawia mikono, pamoja na maji yenye mchanganyiko wa vitu vingine vyenye asili ya kemikali au visivyo na kemikali;

Sura ya 323

"mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Misitu;

"mazingira" maana yake ni masuala yote yanayohusisha maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia ya nchi, sauti, mwanga, harufu, radha, vijiumbe, hali za

kibaiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na binadamu na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana;

"mgahawa wa nje ya jengo" maana yake ni shughuli zote za uuzaji wa chakula na vinywaji zinazofanyika katika sehemu ya nje ya jengo maalum la mgahawa au hoteli;

"mifugo" maana yake ni wanyama wote wafugwao na binadamu kama vile mbwa, ng'ombe, punda, nguruwe, mbuzi, kondoo na kuku;

"misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 na miti, uoto wa asili au uliopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota au ambayo itajumuisha na yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangaza chini ya sheria za misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

Sura ya 191

"mkaguzi wa mazingira" maana yake ni afisa aliyepewa dhamana ya ukaguzi wa mazingira kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tabora pamoja au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki" maana yake ni mtu yeyote ambaye ana miliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala

wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote ndani ya eneo la Halmashauri;

"mzalishaji wa taka" maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara, kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake huzalisha taka ngumu;

"pipa la taka" maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;

"taka" maana yake ni kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani kwa wakati huo na uwepo wake katika eneo hilo unaweza kusababisha chukizo la kiafya na kuhatarisha afya ya jamii;

"taka ngumu" maana yake ni kitu chochote ambacho kinaoza au kutooza baada ya kutumika;

"taka za viwandani" maana yake ni taka maji au taka ngumu zitokanazo na shughuli za viwandani;

"tathmini ya athari kwa mazingira" maana yake ni uchunguzi wa hatua unaofanywa kubaini iwapo programu, shughuli, au mradi utakuwa na madhara kwenye mazingira;

"utapiamlo" maana yake ni hali ya kupungua au kuzidi kwa baadhi ya virutubishi mwilini ambapo husabisha lishe duni au unene uliozidi

"utapiamlo mkali" maana yake ni aina ya utapia mlo uliokithiri ambapo mtu huwa na upungufu mkubwa au kuzidi kwa kiwango kikubwa kwa baadhi ya virutubishi mwilini;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa.

## SEHEMU YA PILI
## WAJIBU WA HALMASHAURI KATIKA USIMAMIZI WA AFYA, USAFI NA MAZINGIRA

Uwezo wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na uwezo wa-
(a) kusimamia utekelezaji wa shughuli za usafi, afya na mazingira;
(b) kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia kanuni za afya, usafi na kutunza mazingira;
(c) kuteua mtu yeyote, wakala, kikundi, taasisi kutekeleza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) kufanya ukaguzi ili kubaini endapo kanuni za afya, usafi na utunzaji wa mazingira zinazingatiwa ndani ya eneo la Halmashauri;
(e) kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtu anayekiuka Sheria Ndogo hii au sheria nyingine inayohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira zilizotungwa na Bunge;
(f) kutunga kanuni, miongozo au kutoa maelekezo yatakayosaidia kulinda afya, usafi na usimamizi wa mazingira ndani ya eneo la Halmashauri; na
(g) kuingia mkataba na mtu yeyote, taasisi au kampuni kutelekeza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira kwa niaba ya Halmshauri katika eneo ndani ya Halmashauri.

Ada ya uzoaji taka

5.-(1) Katika kufanikisha utekelezaji wa usimamizi wa mazingira, Halmashauri itatoza ada ya taka kwa biashara na huduma mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Halmashauri itatoza ada ya taka katika makazi kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Pili.

Uteuzi wa Wakala

6. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala wa kukusanya ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa Wakala

7. Wakala aliyeteuliwa chini ya kanuni ya 6 atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya ada kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) kukusanya ada kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri; na
(c) kutekeleza masharti ya mkataba.

## SEHEMU YA TATU
## USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

8. Mkazi, mfanyabiashara au mmiliki wa jengo au eneo la biashara atahakikisha-

(a) majani yanayozunguka jengo lake yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote kuanzia mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake;
(b) taka ngumu zote ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zinakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na

Halmashauri;

(c) maji taka yanaelekezwa ndani ya mfumo wa maji taka;

(d) anaboresha na kupaka rangi ya jengo lake kila inapochakaa;

(e) ana choo kilicho bora na kisafi wakati wote;

(f) anashiriki siku ya usafi ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi;

(g) anaondoa uchafu ikiwemo mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo katika mifereji ya maji ya mvua inayomzunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mifereji hiyo inakuwa safi wakati wote;

(h) anaweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analotumia kwa shughuli yoyote na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku; na

(i) hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, taka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuathiri upitishaji wa maji ya mvua na hivyo kuruhusu uwepo wa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla.

Biashara ya miwa na matunda

9. Mfanyabiashara wa matunda au miwa atahakikisha kuwa ana chombo maalumu cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.

Marufuku ya upuliziaji dawa bila cheti na kibali

10. Mtu yeyote hataruhusiwa kuendesha biashara ya upuliziaji dawa au biashara ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba au mahali popote bila kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali

na awe amepata kibali kutoka Halmashauri.

Matengenezo ya magari, pikipiki, mitambo na kuegesha magari mabovu

11.-(1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2) Mtu yeyote haruhusiwi-

(a) kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo;

(b) kuegesha magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi au barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo;

(c) kufanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

Udhibiti wa ubebaji kokoto, mawe na mchanga

12.-(1) Mtu yeyote anayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha kimefunikwa ili kuzuia kumwagika na kuchafua mazingira.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi bila kuwa na kibali cha madini.

Ufuaji wa nguo

13. Mtu yeyote anayefanya biashara ya kufua nguo atatakiwa kupata hati ya usafi kabla ya kuanza biashara hiyo.

## SEHEMU YA NNE
## USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kulinda na kutunza vyanzo vya maji

14.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kusimamia na kulinda vyanzo vya maji;

(b) kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji, kuchafua chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi; na

(c) kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya kitaalamu.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa-

(a) kunawa, kuoga, kufua nguo au kunywesha mifugo karibu au kwenye chanzo cha maji kama vile chemchemi, kisima au chanzo kingine chochote cha maji;

(b) kujenga boma la mifugo karibu au kuruhusu mkojo au maji machafu kutoka katika boma la mifugo kuelekea kwenye au karibu na chanzo cha maji kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(c) kufuga mifugo ya aina yoyote bila kibali cha Halmashauri, kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuzurura ovyo mitaani, barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiroruhusiwa;

(d) kuanzisha na kufanya shughuli za aina yoyote ndani ya mita 60 ya maeneo yote oevu na chepechepe kama vile mto na maeneo yote kama ukanda wa kijani;

(e) kulima, kukata miti au kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kujenga au kufanya jambo lolote linaloharibu

kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira;

(f) kumiliki eneo la chanzo cha maji cha asili isipokuwa Halmashauri;

(g) kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai;

(h) kuunganisha maji ya mvua na maji taka au kutapisha choo na kutiririsha vinyesi vya mifugo au binadamu kwenye chanzo cha maji au mfereji wa maji ya mvua; na

(i) kuweka kitu chochote chenye sumu kwenye chanzo cha maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe hai.

Kuchoma au kusababisha moto

15.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa-

(a) kuchoma moto kwa namna yoyote ile katika eneo lolote la Halmashauri;

(b) kuchoma taka ndani ya eneo la Halmashauri; au

(c) kuandaa shamba kwa njia ya kuchoma moto.

(2) Endapo moto mkubwa utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka na kuhamasisha wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto endapo atatakiwa kufanya hivyo na kama atashindwa kushiriki katika zoezi la kuzima moto bila sababu za msingi atakuwa ametenda kosa.

Uchafuzi wa anga hewa kwa moshi

16. Mtu yeyote, mfanyabiashara, hospitali, taasisi, kaya, jengo au shughuli za viwanda haziruhusiwi kuchafua anga hewa kwa kuachilia moshi angani unaoweza kuleta madhara kwa binadamu, mimea na viumbe hai.

Ukataji miti

17-.(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kukata miti katika eneo la Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kibali.

(2) Halmashauri itahakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali ya Taifa.

(4) Mtu yeyote anayetaka kuvuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, mbao au kuni atatakiwa kuwa na eneo maalumu lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kazi hiyo.

Wajibu wa kupanda miti

18.-(1) Kila mkazi ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kupanda na kutunza miti katika eneo lake la makazi au shamba analomiliki.

(2) Kila mmiliki wa jengo la makazi au biashara atawajibika kutunza na kupanda miti katika eneo hilo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kukata miti isipokuwa kwa kibali cha Halmashauri.

Uhifadhi na utunzaji bustani za Halmashauri

19. Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya biashara yoyote au kujenga kitu chochote katika eneo la bustani zote za Halmashauri.

Ushirikishaji

20. Mkurugenzi anaweza kutoa kibali kwa mtu

wa jamii katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira

yeyote, taasisi, kikundi binafsi au asasi ya kiraia, ndani ya Halmashauri katika ngazi ya mtaa, kata au wilaya katika kuboresha bustani, eneo la wazi, kusimamia uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Tathimini ya athari kwa mazingira na jamii

21. Miradi yote inayotekelezwa ndani ya Halmashauri haitaaendelezwa bila kufanyiwa tathmini ya athari ya mazingira.

Udhibiti wa kelele kwa shughuli mbalimbali za kijamii

22. Mtu yeyote hataruhusiwa kusababisha au kufungulia kelele kupita kiasi iwe muziki, kelele za kiwanda, jenereta au kitu kingine chochote bila kibali cha afisa mwidhiniwa.

Makosa yanayotokana na uharibifu wa misitu

23. Mtu yeyote atakuwa anatenda kosa ikiwa-

(a) atachoma au kusababishia moto misitu bila ya kibali;
(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto;
(c) atavuna mazao ya miti katika misitu iliyohifadhiwa bila kibali;
(d) atachoma mkaa au kukata kuni bila kibali;
(e) atafyeka nyasi au kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;
(f) atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti au misitu iliyohifadhiwa kama bustani ya mtu;
(g) atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;
(h) atabandua magome ya miti kwa ajili ya kueneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila kuwa na vibali; au
(i) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu

nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

## SEHEMU YA TANO
## USIMAMIZI WA AFYA YA MAZINGIRA

Usalama wa maji ya kunywa

24. Kila mkazi ana wajibu wa kuhakikisha kwamba maji yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

Usalama wa maji ya visima

25. Kila mmiliki wa kisima ana wajibu wa kuhakikisha maji ya kisima yamepimwa ili yawe salama kwa matumizi.

Utengenezaji, na uuzaji wa vyakula

26. Mtu yeyote hataruhusiwa kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba mpaka bila kuzingatia masharti na kanuni za afya na kupata kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.

Uuzaji wa vyakula vilivyopikwa

27. Kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa ana wajibu wa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

Usalama wa vyakula

28.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuuza vyakula visivyopikwa kwa kuviweka chini.

(2) Mtu anayeuza vyakula visivyopikwa atapaswa kuviweka juu ya meza.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kupanga vyakula nje ya duka la vyakula.

Uzuiaji wa shughuli mbalimbali wakati wa magonjwa ya mlipuko

29. Afisa Mwidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko au kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wakati wa zuio

30.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kumkamata mtu yeyote ambaye atakaidi amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo mtu aliyekamatwa alikuwa anauza vyakula ambavyo vinaharibika kwa haraka Halmashauri itaharibu vyakula hivyo.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) na (2), endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka, Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea kutokana na uharibifu isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa afisa wa Halmashauri au wakala.

Machinjio na maduka ya nyama

31.-(1) Kila mmiliki wa duka la kuuza nyama ana wajibu kuhakikisha kwamba duka lake-

(a) ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa kuweka sakafuni na ukutani marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu;
(b) lina maji safi na misumeno ya kukatia nyama;
(c) lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na sehemu za mizani;

(d) lina pipa la kuhifadhia takataka;na

(e) lina mavazi maalumu kwa ajili ya kuendeshea biashara ikiwemo aproni, mabuti meupe na kofia.

(2) Muuzaji yeyote wa nyama atatakiwa kuvaa vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe na atapaswa kuwa anapima afya kila baada ya miezi sita.

Uchinjaji na uuzaji wa nyama mahali pasiporuhusiwa

32. Mtu yeyote hataruhusiwi kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.

Uendeshaji wa biashara ya nyumba za kulala wageni na hosteli

33.-(1) Kila mmiliki wa nyumba za kulala wageni na hosteli au nyumba ya biashara ana wajibu wa kuhakikisha anapata kibali kutoka Halmashauri kabla ya kuanza biashara.

(2) Endapo mmiliki wa nyumba ya kulala wageni, hosteli au nyumba ya biashara hajakidhi masharti ya kiafya, Halmashauri inaweza kuzuia kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, hosteli au nyumba ya kulala hadi mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti yaliyotolewa na Halmashauri.

Mahitaji ya nyumba ya kulala wageni na hosteli

34. Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, hoteli au hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa katika majengo hayo kuna-

(a) mwanga na hewa ya kutosha;

(b) nafasi na vifaa ama samani za kutosha;

(c) mfumo wa kuaminika wa uondoshaji wa maji taka na taka ngumu;

(d) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;

(e) vyoo na mabafu kwa ajili ya watumiaji wa

jinsi zote;

(f) vifaa vya zima moto;

(g) tanki la kuhifadhia maji safi;

(h) vyoo na bafu vilivyosakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita kutoka usawa wa sakafu.

(i) jozi zaidi ya mbili za mashuka, foronya za mito na magodoro kwa kila kitanda na ziwe na rangi isiyoficha uchafu;

(j) sehemu maalumu ya kufulia na kuanikia nguo; na

(k) stoo na chumba cha kubadilishia nguo kwa ajili ya wafanyakazi.

Upimaji wa afya

35.- Kila mfanyakazi wa hoteli, gereji, saluni, kiwanda, wazoa taka, choo cha umma, mgahawa, baa, bucha, sehemu ya kuokea mikate, nyumba ya kulala wageni, mfagiaji wa barabara au duka la kuuzia pombe ana wajibu wa kupima afya kila baada ya miezi sita katika kituo cha Serikali au kituo cha afya kilichoteuliwa na Halmashauri.

Mamlaka ya kukagua

36. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika jengo lolote wakati wowote wakati wa saa za kazi na wakati wowote inapotakiwa kufanyika kwa ukaguzi maalumu kwa madhumuni ya kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Kufungwa kwa jengo la biashara lisilokidhi masharti ya afya

37. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Ada ya ukaguzi wa afya

38. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara ambayo viwango vyake vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Muda wa kulipa ada

39.-(1) Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha wa Halmashauri, yaani mwezi Julai.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada katika kipindi cha miezi miwili baada ya mwaka wa fedha kuanza atawajibika kulipa kiwango hicho pamoja na adhabu ya asilimia hamsini ya kiwango anachodaiwa.

## SEHEMU YA SITA
## UDHIBITI WA TAKA NGUMU

Udhibiti wa utupaji wa taka

40.-(1) Mtu yeyote haruhusiwi kutupa taka ovyo katika maeneo ya makazi, biashara, mifereji ya maji ya mvua, hifadhi ya barabara au mahali popote pasipotengwa kwa ajili ya kutupa taka.

(2) Watumiaji wa vyombo vya usafiri binafsi au vya umma hawaruhusiwi kutupa taka nje ya vyombo wanavyotumia na taka zote zitawekwa kwenye chombo cha kuhifadhia taka kilichomo kwenye chombo cha usafiri husika.

(3) Mtu yeyote au mkazi ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalumu vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalumu yaliyotengwa.

Wajibu wa kuwa na pipa la taka

41.-(1) Kila mmiliki wa nyumba, mpangaji au mfanyabiashara ana wajibu wa kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhia

taka ngumu kabla hazijachukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa katika eneo lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka.

(2) Kila mmiliki wa nyumba, mpangaji au mfanyabiashara ana wajibu wa kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu na kinatumika kwa kazi hiyo na anakitunza na kukilinda.

(3) Kila mkazi au mtu yeyote ana wajibu wa kutunza na kuhifadhi vyombo vya kuhifadhia taka vinavyowekwa na Halmashauri.

Uanzishwaji wa Vikundi Jamii

42. Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Uhifadhi wa maji taka

43.-(1) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

(2) Mtu yeyote haruhusiwi kufungulia na kutiririsha maji taka au kinyesi kutoka chooni au sehemu yoyote wakati wa mvua au wakati wowote kwenye mifereji ya maji ya mvua, mabonde au maji yanayotembea au sehemu nyingine yoyote isiyoruhusiwa.

Kutiririsha maji taka

44. Mtu yeyote haruhusiwi kutiririsha au kuelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.

Taka za viwanda

45.-(1) Kiwanda chochote hakiruhusiwi kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu,

harufu mbaya, vumbi au kelele na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo la Halmashauri.

(2) Kila mwenye kiwanda ana wajibu wa kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine.

Kaya au jengo la biashaara kulipa ada ya uzoaji taka

46.-(1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kutoka kwa kila kaya, mwenye jengo la biashara au taasisi yoyote.

(2) Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya kieletroniki yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(3) Endapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

(4) Bila kuathiri kanuni ya 16 cha Sheria Ndogo hii ni marufuku kwa mtu yeyote, kampuni, wakala au taasisi kuendesha shughuli za uchomaji wa taka hatarishi bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

## SEHEMU YA SABA
## UJENZI NA MATUMIZI YA VYOO

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

47.-(1) Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji ana wajibu wa kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi na imara kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo.

(2) Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji ana wajibu wa kuweka sehemu maalumu ya kunawa mikono yenye maji safi na sabuni ya kimiminika.

Umbali wa kujenga choo

48. Choo chochote kinapaswa kujengwa umbali wa mita sitini kutoka chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani.

Vyoo vya umma

49.-(1) Halmashauri inaweza kujenga choo cha umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga choo cha umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona inafaa.

(2) Vyoo vitakavyojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitatakiwa kuwa vya kudumu na viwe na-

(a) matundu yasiyopungua mawili kwa wanawake na mawili kwa wanaume;
(b) mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama;
(c) chombo cha kuhifadhia maji ya akiba;
(d) bafu ya wanaume na wanawake;
(e) sehemu ya haja ndogo kwa wanaume; na
(f) chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

50. Mtu yeyote, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano, sherehe au mkusanyiko wowote ina wajibu wa kuweka au kujenga choo cha muda endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu na itatakiwa kuomba idhini kutoka Halmashauri.

Vyoo katika majengo ya biashara

51. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hii kwa ajili ya matumizi ya wateja wake kwa kuzingatia jinsi zote.

Ilani ya

52. Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika

kujenga au kurekebisha choo

kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

Kufungwa kwa jengo

53. Bila kuathiri masharti ya kanuni ya 54, Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo lisilo na choo au lenye choo kisichofaa kwa matumizi lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa.

Ilani ya kuondoa kero

54.-(1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote, atatoa ilani ndani ya siku saba kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa anatenda kosa.

Eneo maalumu la uvutaji sigara

55.-(1) Mtu yeyote haruhusiwi kuvuta sigara kwenye eneo la wazi au kwenye mikusanyiko ya watu.

(2) Kila mwenye jengo la biashara za baa, hoteli, mgahawa, kumbi za starehe, viwanja vya michezo na burudani, ofisi za umma na binafsi anatakiwa kutenga eneo maalumu la kuvutia sigara na kuweka chombo cha kuhifadhia majivu na vichungi vya sigara.

Ukaguzi wa afya

56. Halmashauri kupitia afisa afya ya mazingira itafanya ukaguzi wa afya kwenye maeneo yote ya makazi, biashara au shughuli yoyote yaliyopo katika eneo la Halmashauri.

## SEHEMU YA NANE
## WAJIBU WA HALMASHAURI KATIKA USIMAMIZI WA LISHE

Wajibu wa Halmashauri ya kijiji au mtaa

57.-(1) Halmashauri ya kijiji au Mtaa itakuwa na wajibu wa-

(a) kushirikiana na wataalamu wa afya na lishe kutoa elimu inayohusiana na masuala ya lishe kwa wananchi;
(b) kuhakikisha taarifa zote zinazohusiana na lishe zinajadiliwa, kufanyiwa uamuzi na zinabandikwa kwenye mbao za matangazo katika Ofisi za kijiji au mtaa husika;
(c) kuhakikisha siku ya afya na lishe inaadhimishwa kwa kila robo mwaka katika mtaa au kijiji;
(d) kuhakikisha watoto wote chini ya miaka mitano wanaogundulika kuwa na utapiamlo mkali wanapelekwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya matibabu;
(e) kuhakikisha watoto wote chini ya miaka mitano wanahudhuria kliniki kulingana na tarehe iliyopangwa na mtoa huduma za afya;
(f) kuhimiza wajawazito kuhudhuria kliniki kwa muda wote wa ujauzito; na
(g) kuhakikisha kila shule inakuwa na utaratibu maalumu wa kuwawezesha watoto kupata mlo wa mchana shuleni.

Wajibu wa wataalamu wa afya na lishe

58.-(1) Mtaalamu wa afya na lishe atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kutembelea kaya na kutoa elimu inayohusu masuala ya lishe;
(b) kufanya utambuzi wa watoto wenye utapiamlo katika mtaa au kijiji;

(c) kutoa taarifa ya masuala ya lishe katika vikao vya Halmashauri ya kijiji;
(d) kumpa rufaa mtoto mwenye utapiamlo kwenda kituo wanachotolea huduma za afya; na
(e) kufanya utambuzi wa hali ya lishe kwa watoto chini ya miaka mitano.

Wajibu wa mzazi au mlezi

59. Kila mzazi au mlezi katika kila kaya atakuwa na wajibu ufuataao:
(a) kuhakikisha mtoto chini ya miaka mitano anapelekwa kliniki;
(b) kuhakikisha mtoto au mjamzito anapewa chakula cha virutubisho kadiri ya maelekezo ya mtaalamu wa lishe au mhudumu wa afya ngazi ya jamii;
(c) kuhakikisha mtoto mwenye utapiamlo anapelekwa kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kupatiwa matibabu ya utapiamlo;
(d) kuhakikisha usafi na usalama wa mji unatekelezwa katika kata;
(e) kuhakikisha mtoto anapewa matone ya nyongeza ya vitamini "A" na dawa za minyoo kwa kadiri ya maelekezo ya mtaalamu wa afya; na
(f) kuhakikisha mjamzito anahudhuria kliniki muda wote wa ujauzito.

Kamati ya Lishe ya Halmashauri

60. Kutakuwa na Kamati ya Lishe ya Halmashauri yenye wajumbe wafuatao:
(a) Mkuu wa Wilaya ambaye atakuwa mwenyekiti wa kamati;
(b) Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye atakuwa katibu wa kamati;

(c) Afisa Utumishi wa Halmashauri;
(d) Mweka Hazina wa Halmashauri;
(e) Mganga Mkuu wa Halmashauri;
(f) Afisa Lishe wa Halmashauri;
(g) Watendaji wa Kata zote zilizomo ndani ya Halmashauri; na
(h) wadau wa maendeleo wanaofanya kazi eneo la Halmashauri.

Wajibu wa Kamati ya Lishe ya Halmashauri

61. Kamati ya Lishe ya Halmashauri itakuwa na wajibu wa-
(a) kufanya tathimini ya utekelezaji wa shughuli za lishe ndani ya Halmashauri;
(b) kuhakikisha kuwa shughuli zinazopaswa kutekelezwa katika ngazi ya mtaa au kijiji zinatekelezwa; na
(c) kuratibu na kuhakikisha kuwa vikao vya tathmini ya lishe katika ngazi ya Halmashauri vinafanyika kila robo mwaka na taarifa inawasilishwa katika Kamati ya Lishe ya Mkoa.

Maeneo ya kutolea huduma ya lishe

62. Mtaalamu wa afya na lishe atatoa huduma ya lishe katika kila kaya na kituo cha kutolea huduma za afya au eneo lolote litakaloainishwa.

Makosa

63. Mtu yeyote atakuwa anatenda kosa endapo-
(a) atamzuia au kujaribu kumzuia au atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) atamwaga taka barabarani, katika mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(c) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;
(d) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;
(e) ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo cha maji au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;
(f) atapika vyakula pembezoni mwa barabara au nje ya majengo mengine;
(g) atauza vyakula maeneo yasiyo rasmi au kushindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;
(h) atafanya matengenezo ya magari, pikipiki au mitambo katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;
(i) atavuta sigara hadharani, mahali pa jumuiya au kwenye vyombo vya usafiri;
(j) atatema mate ovyo au kutema mate barabarani au mahali pa jumuiya;
(k) ataacha nyumba anayoishi, anayomiliki au anayofanyia shughuli zake katika hali ya uchafu yenye kuleta kero au chukizo;
(l) ataacha chombo cha usafiri katika hali ya uchafu;
(m) ataendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;
(n) ataanzisha au kufungua karakana katika

majengo, majumba au maeneo ya makazi;

(o) ataenda haja ndogo au kubwa barabarani, uchochoroni, upenuni au mahali popote ambapo si chooni;

(p) atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali kutoka Halmashauri;

(q) atafanya mikusanyiko wakati wa mlipuko wa magojwa ya kuambukiza bila idhini ya Halmashauri; au

(r) atapanda mazao yenye urefu wa kuzidi sentimita thelathini katika kata ya Cheyo, Ipuli, Tambukareli, Mpela, Kidongo Chekundu, Kiloleni, Isevya, Kanyenye, Kitete, Mbugani, Ng'ambo, Gongoni, Chemchem, Mapambano na Mwinyi.

Adhabu

64. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili.

Kufifilisha kosa

65. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii, kiasi kisichozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoanishwa kwenye Jedwali la Nne.

Kufutwa kwa Ts Na. 361 la 2015

66. Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za mwaka 2015 zimefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 5(1))*

ADA YA UZOAJI WA TAKA

| Namba | Aina ya Makazi | Kipato cha chini kwa mwezi |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za ghorofa usanifu wa kawaida(Kwa kaya) | 2,000 |
| 2 | Nyumba za chini(kwa kaya) | 2,000 |
| 3 | Nyumba mpya za ghorofa usanifu wa kawaida | 3000 |
| 4 | Nyumba mpya za ghorofa usanifu wa kisasa | 5,000 |
| 5 | Nyumba ya pekee(Bungalow) | 5000 |
| 6 | Nyumba ya pekee yenye nyumba za huduma (Villa) | 8000 |

| Namba | Aina ya mzalishaji wa taka | Kiwango cha ada kwa mwezi |
|---|---|---|
| | | Kipato cha chini |
| 8 | Hostel (kwa mpangaji /mkazi ) | 500 |
| 9 | Hostel (kwa chumba) | 2000 |
| 10 | Nyumba ya kulala wageni | 10000 |
| | OFISI | |
| | • Ofisi - 1 – 10 wafanyakazi | 10,000 |
| | • Ofisi – 11 – 50 wafanyakazi | 15,000 |
| | • Ofisi – 51 – 100 wafanyakazi | 20,000 |
| | • Ofisi – 101 – zaidi ya wafanyakazi | 50,000 |
| | BENKI | |

| | | |
|---|---|---|
| 11 | Tawi la Benki ya biashara | 20,000 |
| 12 | Duka la kubadilishia fedha | 20,000 |
| 13 | Ofisi za ATM | 20,000 |
| 14 | Ofisi za luku (Tanesco) | 12,000 |
| 15 | Ofisi za luku(wakala) | 51,000 |
| | Mawakala wa fedha kwa mitandao ya simu na benki | 15,000 |
| | VYAKULA NA VINYWAJI | |
| 16 | Sehemu ya kutengenezea chai na vitafunwa | 10,000 |
| 17 | Cafe/Restaurant | 10,000 |
| 18 | Duka la vyakula na vinywaji | 10,000 |
| 19 | Baa( pombe, vinywaji baridi na vitafunwa) | 10,000 |
| 20 | Mama na baba lishe | 5,000 |
| 21 | Taka zinazotokana na Biashara ya Mgahawa wa nje ya Majengo | 10,000 |
| 22 | Vibanda vya chips | 5000 |
| 23 | Baa na mgahawa/jiko | 5,000 |
| 24 | Baa na nyumba ya kulala wageni | 20,000 |
| 25 | Baa, nyumba ya wageni na Ukumbi wa starehe | 10,000 |
| 26 | Baa na ukumbi wa starehe | 10,000 |
| 27 | Baa, Ukumbi wa starehe na mgahawa | 10,000 |
| 28 | Ukumbi wa starehe | |
| | Watu 01 hadi 300 | 70,000 |
| | Watu 301hadi750 | 80,000 |
| 29 | Duka la kuuza *Ice Cream* | 10,000 |
| 30 | HOTELI | |
| | 10 Vyumba | 30,000 |
| | 11- 20 Vyumba | 50,000 |
| | 21- 30 Vyumba | 50,000 |
| | 31- 40 Vyumba | 50,000 |
| | 41- 50 Vyumba | 60,000 |
| | 51- 70 Vyumba | 70,000 |
| | 71- 100 Vyumba | 80,000 |
| | 101- Na kuendelea | 90,000 |
| 31 | BUCHA YA NYAMA NA SAMAKI WABICHI | 5,000 |
| | DUKA ( JUMLA NA REJA REJA) | |
| 32 | Vyakula/Bidhaa mchanganyiko | 10,000 |
| 33 | Duka la Nguo | 5,000 |
| 34 | Vifaa vya umeme au simu (Electronic phone, | 8,000 |

| | | |
|---|---|---|
| | phone accessories and electrical appliances) | |
| 35 | Vifaa vya ujenzi Hardware/ Machinery | 15,000 |
| 36 | Vitabu/ Shajala | 5,000 |
| 37 | Urembo/ Vipodozi | 5,000 |
| 38 | Duka la Samani (Furniture and Machinery) | 10,000 |
| 39 | Vinywaji na Pombe Kali (beverages and liquor stores) | 5,000 |
| 40 | Taka zinazotokana na ghala la kuhifadhia bidhaa (Store ) | 10,000 |
| 41 | Vipuri na Vifaa (Spare parts and tools) | 10,000 |
| 42 | Duka la Vifaa Chakula | 10,000 |
| | KARAKANA NA VIWANDA | |
| 43 | Fundi Seremala | 10,000 |
| 44 | Karakana ya Chuma (Metal W/ shops) | 10,000 |
| 45 | Karakana ya Magari (Motor Garage) | 20,000 |
| 46 | Karakana ya pikipiki (motocycle gerage) | 15000 |
| 47 | Sonara na uhunzi wa vito (Jewerly and Black Smith) | 5000 |
| 48 | Shughuli za Vioo (Glass Works)/ Shughuli za Alminium | 10,000 |
| 49 | Mchapishaji | 20,000 |
| 50 | Stoo | 20,000 |
| 51 | Mashine ya Mbao kwa ujazo wa mita moja (saw mill per meter cubic) | 15,000 |
| | VIWANDA VIDOGO NA VIKUBWA | |
| 52 | Kwa tani moja ya taka kwa ujazo mkubwa | 25,000 |
| 53 | Kwa ujazo wa mita moja cubic meter | 25,000 |
| 54 | Umeme na Matengenezo ya Elektroniki (Electronical anad Electronic repair) | 10,000 |
| 55 | Magurudumu na Matengenezo | 10,000 |
| | BIASHARA NDOGO NA NYINGINEZO | |
| 56 | Fundi Cherehani | 5,000 |
| 57 | Seremala | 5,000 |
| 58 | Fundi viatu | 2,000 |
| 59 | Saluni ya Nywele | 5,000 |
| 60 | Dobi | 5,000 |
| 61 | Genge kwa meza moja | 2,000 |
| 62 | Biashara ya juisi ya miwa | 10,000 |
| 62(a) | Wauza matunda na juisi nyinginezo | 5,000 |
| 62(b) | Wafanyabiashara wadogo wasio na maeneo maalum. | 500 kwa siku |

*Tangazo La Serikali Na. 320 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 63 | Huduma za Internet | 3,000 |
| | HUDUMA ZA AFYA (TAKA ZISIZOKUWA ZA HATARI) | |
| 64 | Duka la dawa baridi | 8,000 |
| 65 | Duka la Dawa Rejareja (Retail Pharmacy) | 5,000 |
| 66 | Duka la Vifaa vya Maabara | 3,000 |
| 67 | Maabara ya Vipimo | 3,000 |
| 68 | Zahanati | 8,000 |
| 69 | Kituo cha Afya | 5,000 |
| 70 | Dawa asilia | 5,000 |
| 71 | Hospitali | 10,000 |
| 72 | Kliniki | 10,000 |
| 73 | Hospitali ya Rufaa | 40,000 |
| | TAASISI ZA MAFUNZO | |
| 74 | Kituo cha kulelea watoto, Shule ya Sekondari, Shule ya Msingi na Vyuo vya Kutwa | |
| | 01- 200 Wanafunzi | 15,000 |
| | 201- 500 Wanafunzi | 30,000 |
| | 501-1,000 Wanafunzi | 30,000 |
| | 1001- na kuendelea | 80,000 |
| 75 | Shule na Vyuo vya Bweni zisizo za serikali | |
| | 02- 200 Wanafunzi | 40,000 |
| | 201- 500 Wanafunzi | 50,000 |
| | 501-1,000 Wanafunzi | 150,000 |
| | 1001- na kuendelea | 80,000 |
| | VITUO VYA MAFUTA | |
| 76 | Kituo kikubwa cha Mafuta(Pump 6+) | 100,000 |
| 77 | Kituo kidogo cha Mafuta (pump 1-5) | 15,000 |
| 78 | Kituo cha Mafuta ya taa | 20,000 |
| 79 | Kituo cha Kuuzia gesi | 30,000 |
| 80 | Kibanda cha Kuuzia mkaa (Kikubwa) | 40,000 |
| 81 | Kibanda cha Kuuzia Mkaa (Kidogo gunia 1- 10) | 30,000 |
| 82 | Msikiti au Kanisa bila ya kuwa na shughuli nyingine za Kibiashara | 20,000 |
| 83 | Msikiti au Kanisa ukiwa na shughuli nyingine za Kibiashara | 50,000 |
| | HUDUMA NYINGINEZO | |
| 84 | Jumba la Starehe/ Klabu/cassino/night clubs | 50,000 |
| 85 | Ofisi za ulinzi | 5000 |
| 86 | Tax kwa siku | 200 |
| 87 | Daladala kwa siku | 500 |
| 88 | Lori la Mizigo kwa siku | 1000 |
| 89 | Minara ya simu na mawasiliano mengine | 8,000 |
| | TAKA ZENYE UJAZO MKUBWA | |

| | | |
|---|---|---|
| 90 | Taka za Bustani kwa Mita Mraba Moja | 5,000 |
| 91 | Taka za Viwandani kwa Tani | 20,000 |
| 92 | Taka za Masoko kwa Tani kwa Mita mraba | 25,000 |
| 93 | Ghala (Godown) kwa mwezi | 30,000 |
| 94 | Duka la Vifaa vya Muziki kwa mwezi | 20,000 |
| 95 | Duka la CD na Cassette kwa mwezi | 5,000 |
| 96 | Bahati nasibu kwa mwezi | 5,000 |
| 97 | Taka za Biashara kwa Tripu (Super market, hyper market na nyinginezo) | 40,000 |
| 98 | Taka za Uvunjaji wa Jengo kwa tani moja (Demolition Debris per ton) | 20,000 |
| 99 | Kituo cha Kuchakata Taka (Recycling Center Plant) kwa mwezi | 10,000 |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2))*

Kaya moja kiwango kwa mwezi Shilingi 3,000

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 18(2))*

UPANDAJI MITI KWA KUZINGATIA MAENEO

| | |
|---|---|
| Ujazo wa juu | Miti isiyo pungua 2 |
| Ujazo wa kati | Miti isiyo pungua 4 |
| Ujazo wa chini | Miti isiyo pungua 5 |

## JEDWALI LA NNE

*(Limetegenezwa chini ya kanuni ya 65)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, kwamba mnamo tarehe ………… ya mwezi…………. Mwaka ……… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ……………ya Sheria Ndogo ya Afya, Lishe na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ya Mwaka 2024.
Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha ada ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.
Leo tarehe …………………..ya Mwezi …………… Mwaka …………………
Jina: …………………………...
Saini: …………………………….

MBELE YANGU:
Jina: ……………………………………
Wadhifa: ……………………………….
Saini: …………………………………..
Tarehe: ………………………………...

Lakari ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufutia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora uliofanyika tarehe 12 mwezi 05 Mwaka 2023 na kushuhudiwa lakari hiyo ikigongwa mbele ya;-

ELIAS MAHWAGO KAYANDABILA
*Mkurugenzi wa Manispaa*
*Halmashauri ya Manispaa ya Tabora*

MHE. RAMADHANI S. KAPELA
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Manispaa Tabora*
/

L.S

NAKUBALI

Dodoma,
20 February, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*